

SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 60 **JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC)** FEBRUARI 2026

KARIBU WALIMU AJIRA MPYA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

✓ **Salamu za Katibu wa Tume ya Utumishi
wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama**



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama.

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania [tumeyautumishiwawalimutanzania](https://www.instagram.com/tumeyautumishiwawalimutanzania)

WALIMU WAPYA NA DHAMANA YA TAIFA

Kuajiriwa kwa walimu wapya ni utekelezaji wa dhamira ya Serikali ya kuimarisha sekta ya elimu na kuwekeza katika rasilimali watu kwa ajili ya maendeleo ya taifa. Hatua hii inalenga kuhakikisha upatikanaji wa elimu bora na endelevu kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Walimu wapya wanaojiunga na utumishi wa umma wamekabidhiwa jukumu kubwa la kitaifa la kufundisha na kuwaandaa wanafunzi kuwa raia wema, wazalendo na wenye mchango chanya katika jamii. Serikali inawataka walimu hawa kutekeleza majukumu yao kwa kujituma, weledi na kuzingatia misingi ya taaluma ya ualimu.

Serikali inasisitiza umuhimu wa walimu kuzingatia maadili, nidhamu na mwenendo kazini na katika jamii.

Maadili mema ni msingi wa kuimarisha heshima ya taaluma ya ualimu na kujenga imani ya jamii kwa walimu.

Walimu wanakumbushwa kusoma na kuelewa Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma pamoja na miongozo ya mbalimbali ili kutambua haki na wajibu wao na kuzingatia taratibu sahihi katika utekelezaji wa majukumu.

Hatimaye, Serikali inatoa wito kwa walimu waliopo shuleni kuwapatia walimu wapya ushirikiano unaohitajika ili waweze kuzoea mazingira ya kazi na kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, kwa lengo la kuendelea kuijenga sekta ya elimu kuwa chachu ya maendeleo ya taifa.

KATUNI



BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti
Paulina M. Nkwama

Wajumbe
Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya
Edwin Mgendera
Apsa Othman
Asha Lubuva

Mhariri Mkuu
Artemony T. Vincent

Mhariri
Adili J. Mhina

Msanifu Kurasa
Lucas G. Ogunde

Wasiliana nasi kwa Simu: +255 782 366 622 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** secretary@tsc.go.tz
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, **S.L.P 353, DODOMA.**



KARIBU WALIMU AJIRA MPYA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

Karibuni sana walimu ajira mpya katika Utumishi wa Umma. Kama mnavyokumbuka, mojawapo ya ahadi za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ndani ya siku 100 za kuwa madarakani, ilikuwa ni kutoa ajira 7,000 za walimu kama sehemu ya jitihada za kuboresha sekta ya elimu nchini.

Kuajiriwa kwenu katika Utumishi wa Umma ni ushahidi tosha kuwa ahadi hiyo imetekelezwa. Kwa niaba ya Tume ya Utumishi wa Walimu, tuna kila sababu ya kumshukuru na kumpongeza Rais kwa juhudi kubwa anazoendelea kuzifanya kwa ajili ya maendeleo ya elimu na taifa kwa ujumla.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeundwa kwa mujibu wa Sheria Sura ya 448. Tume hii ni Mamlaka ya Ajira na Nidhamu kwa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari walio katika Utumishi wa Umma Tanzania Bara. TSC ina ofisi katika ngazi ya Wilaya na Makao Makuu. Wilaya zote 139 za Tanzania Bara zina ofisi za Tume na ofisi moja (1) ni Makao Makuu ambayo ipo Mtaa wa Mtendeni, jijini Dodoma.

Napenda kuwapongeza kwa kufanikiwa kujiunga na taaluma ya ualimu kupitia ajira ya Serikali. Hii ni hatua kubwa na ya heshima, kwani mmeingia katika wito wa kitaifa wa kuunda na kulea kizazi cha kesho.

Taifa limewaamini na kuwapa dhamana kubwa ya kuwahudumia watoto wake kupitia elimu. Dhamana hii imelenga kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu bora, wanakuwa raia wema, na wanajengewa misingi ya weledi, maadili na uzalendo.

Mmechaguliwa kwa kuzingatia uwezo, bidii na sifa zenu za kitaaluma. Sasa ni jukumu lenu kuthitisha kuwa Serikali haijakosea kuwapa dhamana hiyo muhimu. Nawasihi mfanye kazi kwa kujituma, weledi na uzalendo.

Ualimu ni kazi ya huduma kwa jamii, siyo tu kufundisha masomo darasani bali ni kazi ya kuunda tabia, kukuza maadili na kuibua vipaji vya watoto. Kupitia kazi yenu, mnachangia moja kwa moja maendeleo ya taifa na mustakabali wa kizazi kijacho.

Maadili na mwenendo bora ni nguzo muhimu katika taaluma ya ualimu. Ninawasihi kuishi katika maadili mema kazini na nje ya maeneo ya kazi. Zingatieni misingi ya uadilifu, heshima, uwajibikaji na uzalendo, mkikumbuka kuwa wanafunzi wanawatazama kama mfano wa kuigwa.

Epukeni vitendo vya ukosefu wa nidhamu, ikiwemo kuchelewa kufika kazini, utoro, ukosefu wa heshima kwa viongozi, mahusiano ya kimapenzi na wanafunzi, adhabu zisizo halali kwa wanafunzi, mikopo isiyoendana na taratibu za Utumishi, pamoja na vitendo vingine vinavyokiuka Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma.

Ni muhimu kwa walimu wapya, pamoja na waliopo kazini, kusoma na kuelewa nyaraka mbalimbali za kiutumishi, ikiwemo Sheria, Kanuni na Miongozo ya Utumishi wa Umma, Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu, Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu Wapya Wanaojiriwa katika Utumishi wa Umma Tanzania Bara, pamoja na miongozo mingine ya Tume. Nyaraka hizi zitawasaidia kutambua haki zenu, wajibu wenu na taratibu sahihi za kuzidai. Nyaraka hizo zinapatikana kupitia tovuti ya Tume: www.tsc.go.tz.

Ninawasihi kuwa na ushirikiano mzuri na walimu mnaowakuta shuleni ili utumishi wenu uwe na tija. Ushirikiano mzuri utasaidia kuleta mazingira mazuri ya kazi, kuimarisha nidhamu, na kuhakikisha utekelezaji bora wa majukumu. Walimu waliopo shuleni pia wanatakiwa



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama.

kuwakaribisha walimu wapya kwa moyo wa uzalendo na kuwasaidia kujifunza utamaduni wa shule, taratibu za kazi, na mbinu za kutoa elimu bora kwa wanafunzi.

Aidha, ninawasihi Wakuu wa Shule, Ofisi za Wakurugenzi wa Mamlakaza Serikali za Mitaa pamoja na viongozi wengine wa ngazi mbalimbali katika halmashauri kuendelea kuwa karibu na walimu kwa kuwapa ushauri, msaada na mazingira rafiki ya kazi, ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa amani na utulivu huku wakiwa na ari ya kufanya kazi.

Kadhalika, ninawaomba wazazi na jamii kwa ujumla kuwapa walimu ushirikiano na heshima wanayostahili, kushirikiana nao katika malezi na maendeleo ya watoto, na kuunga mkono juhudi zao za kutoa elimu bora. Ushirikiano huu ndio msingi wa mafanikio ya elimu na ujenzi wa taifa lenye maarifa na maadili mema.

Nawapongeza tena kwa kujiunga na Utumishi wa Umma. Karibuni sana. Kazi na Utu Tunasonga Mbele.

SAUTI ZA WALIMU ZATHIBITISHA JUHUDI ZA SERIKALI KATIKA KUBOresha HUDUMA KWA WALIMU



Mwl. Richard Joseph Yilika, mwalimu wa Shule ya Sekondari Makoko, Musoma, mwenye uzoefu wa miaka 21 kazini, akizungumza kuhusu maboresho ya maslahi ya walimu chini ya Serikali ya Awamu ya Sita.

Na Mwandishi Wetu Maalum

Sekta ya elimu nchini Tanzania imeendelea kushuhudia mageuzi makubwa tangu kuingia madarakani kwa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mageuzi hayo yamegusa moja kwa moja maslahi ya walimu, mazingira ya kazi, miundombinu ya shule, ajira, matumizi ya teknolojia pamoja na utekelezaji wa mitaala mipya inayolenga elimu ya ujuzi na vitendo.

Kupitia mahojiano maalum yaliyofanyika na walimu kutoka shule za msingi na sekondari katika Mkoa wa Mara, walimu hao wamesema bila kusita kuwa jitihada

za Serikali zinaonekana wazi na zimeleta matumaini mapya kwa walimu waliokuwa wamekata tamaa kutokana na changamoto za muda mrefu.

Walimu walioshiriki ni pamoja na Mwl. Richard Joseph Yilika wa Shule ya Sekondari Makoko, Musoma (uzoefu wa miaka 21), Mwl. Jacobo Luzama Revocatus wa Shule ya Msingi Taramoroni, Tarime (miaka 20), Mwl. Tabitha Mabula Kilyabumu wa Shule ya Msingi Ingrijuu, Rorya (miaka 20), Mwl. Mussa Kaswahili Raphael wa Shule ya Msingi Kambarage, Serengeti (miaka 22) pamoja na Mwl. Maliki Melckiad Raphael wa Shule ya Sekondari Morotonga, Serengeti (miaka 13).



Mwl. Jacobo Luzama Revocatus, mwalimu wa Shule ya Msingi Taramoroni, Tarime, mwenye uzoefu wa miaka 20, akielezea manufaa ya upandishwaji wa madaraja na ajira mpya za walimu.

Maboresho ya Maslahi: Walimu Warejeshewa Imani na Motisha

Akizungumzia maboresho ya maslahi ya walimu, Mwl. Richard Yilika amesema Serikali imechukua hatua madhubuti zilizogusa moja kwa moja maisha ya walimu, hasa katika mishahara na madaraja.

“Serikali imefanya maboresho makubwa ya maslahi ya walimu, hususan mishahara na upandishwaji wa madaraja kwa mserekeru kwa waliokuwa na changamoto. Nyongeza ya mishahara ya kila mwaka iliyokuwa imesimama kwa muda mrefu sasa tunaona. Tunashukuru sana Serikali kwa kutujali,” amesema Mwl. Yilika.

Kauli hiyo inaakisi hali ya walimu wengi waliokuwa wamekwama katika madaraja kwa muda mrefu bila mabadiliko yoyote, hali iliyokuwa ikishusha morali ya kazi.

Kwa upande wake, Mwl. Jacobo Revocatus amesema ingawa kwa kipindi kifupi lakini anaona mabadiliko makubwa.

“Tunakiri, kuna kitu kimefanyika,” amesema, kauli ambayo imebeba uzito mkubwa kutokana na uzoefu wake wa miaka mingi kazini.

Kunufaika Binafsi: Malalamiko Yapungua, Haki Zarejeshwa.

Walimu wengi wameeleza kunufaika moja kwa moja na hatua zilizochukuliwa na Serikali tangu mwaka 2021. Mwl. Revocatus amesema alicheleweshwa kupandishwa daraja kwa miaka nane tangu mwaka 2013, jambo lililokuwa



Mwl. Tabitha Mabula Kilyabumu, mwalimu wa Shule ya Msingi Ingrijuu, Rorya, mwenye uzoefu wa miaka 20, akizungumza juu ya motisha ya kazi na uboreshaji wa mazingira ya ufundishaji.

SAUTI ZA WALIMU ZATHIBITISHA JUHUDI ZA SERIKALI KATIKA KUBOresha HUDUMA KWA WALIMU



Mwl. Mussa Kaswahili Raphael, mwalimu wa Shule ya Msingi Kambarage, Wilaya ya Serengeti, mwenye uzoefu wa miaka 22, akieleza mchango wa miundombinu bora katika kuongeza ufanisi wa ufundishaji.

Mwl. Maliki Melckiad Raphael, mwalimu wa Shule ya Sekondari Morotonga, Wilaya ya Serengeti, mwenye uzoefu wa miaka 13, akifafanua faida za matumizi ya TEHAMA na ulipaji wa mishahara kwa wakati.

likimkatisha tamaa.

"Nilikuwa nalalamika sana kwa sababu nilikaa muda mrefu bila kupanda daraja. Lakini sasa mambo yamekaa sawa kabisa, sina malalamiko tena," amesema kwa furaha.

Naye Mwl. Tabitha Mabula amesema kupata mserekeo na kubadilishiwa cheo kulimpa hamasa mpya kazini.

"Baada ya mserekeo nimebadilishiwa cheo, hali hii imenipa motisha ya kufanya kazi kwa bidii zaidi," amesema.

Kwa Mwl. Maliki Melckiad, ufanisi wa mifumo ya kiutumishi umeondoa usumbufu uliokuwepo zamani.

"Mara baada ya kuhitimu masomo, nilipowasilisha maombi, nilibadilishiwa cheo bila kuchelewa. Hii ni tofauti kabisa na ilivyokuwa zamani," amesema.

Ajira Mpya na Miundombinu: Suluhisho la Uhaba na Msongamano

Katika eneo la ajira, walimu wamesema Serikali imefanya kazi kubwa ya kuajiri walimu wapya, hali iliyopunguza uhaba uliokuwepo kwa miaka mingi.

Mwl. Revocatus amesema shule yao imepokea zaidi ya walimu 10 kwa kipindi hiki cha Serikali ya Awamu ya Sita.

"Hatua hii imetupunguzia mzigo mkubwa wa kazi na kuboresha ufundishaji," amesema.

Mwl. Mussa Kaswahili amesema pamoja na ajira, Serikali imewekeza kwa kiasi kikubwa kwenye miundombinu ya elimu.

"Kuna ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu na vyoo. Miundombinu hii imepunguza msongamano wa wanafunzi na kutupa mazingira tulivu ya kazi," amesema.

Naye Mwl. Maliki amesema miundombinu bora imechochea ongezeko la wanafunzi wanaoandikishwa shuleni, jambo linaloonesha imani ya jamii kwa mfumo wa elimu.

Tehama: Mapinduzi ya Utendaji Kazi

Matumizi ya mifumo ya TEHAMA yameelezwa kuwa mkombozi mkubwa kwa walimu. Mwl. Yilika amesema mifumo hiyo inaokoa muda na kuondoa usumbufu wa kuzunguka ofisi mbalimbali kutafuta huduma.

"Kupitia TEHAMA, taarifa zinafika kwa wakati na hakuna upotevu. Inatusaidia kubaki vituoni badala ya kuzunguka," amesema.

Kupitia mradi wa BOOST, walimu wameanza kutumia madarasa janja, huku mifumo mbalimbali ikirahisisha tathmini ya utendaji kazi, uhamisho wa wanafunzi na hata upatikanaji wa mikopo.

Mtaala Mpya: Elimu ya Ujuzi na Vitendo

Walimu wamepongeza utekelezaji wa mitaala mipya inayolenga elimu ya vitendo. Wamesema mitaala hiyo inamwandaa mwanafunzi kujitegemea na kukabiliana na mahitaji ya dunia ya sasa.

Hata hivyo, wametoa mapendekezo kwa Serikali kuendelea kuwawezesha walimu kupitia mafunzo endelevu, kuajiri zaidi na kujenga miundombinu kama maabara za TEHAMA na karakana.

Maadili na Uongozi Shuleni

Akizungumza kama Mkuu wa Shule, Mwl. Tabitha Mabula amesema maadili ya walimu yako katika hali nzuri, huku changamoto chache zikishughulikiwa kupitia vikao vya mara kwa mara.

"Tunakumbushana na kushauriana umuhimu wa kuzingatia maadili ya kazi," amesema.

Hitimisho

Kwa ujumla, sauti za walimu hawa zinathibitisha kuwa jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita zimeleta mageuzi ya kweli katika sekta ya elimu. Maboresho ya maslahi, ajira, miundombinu, TEHAMA na mitaala mipya yameongeza motisha, ufanisi na heshima ya taaluma ya ualimu.

Walimu wameahidi kuendelea kushirikiana na Serikali kwa bidii na uzalendo, wakiadini kuwa uwekezaji unaofanywa leo ndio msingi wa kujenga taifa lenye wasomi, wataalam na raia wanaojitegemea kesho.

TSC TARIME YANG'ARA: WALIMU ZAIDI YA 3,000 WAPANDISHWA VYEO NDANI YA MIAKA MINNE

Na Mwandishi Wetu, Tarime

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Tarime imeendelea kuandika historia ya mafanikio katika kusimamia ajira, maadili na maendeleo ya walimu, baada ya kuonyesha matokeo chanya makubwa kati ya mwaka 2021 na 2025.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Tarime, Bw. Agutu Julius, ofisi hiyo imepiga hatua kubwa katika kuimarisha ustawi wa walimu wa shule za msingi na sekondari, hususan katika eneo la upandishwaji vyeo.

Bw. Julius alisema kuwa jumla ya walimu 3,099 wamepandishwa vyeo katika kipindi cha miaka minne, huku baadhi yao wakipanda zaidi ya cheo zaidi ya mara moja, hatua inayodhihirisha uwajibikaji na ufanisi wa Tume hiyo.

"Upandishwaji vyeo umefanyika kwa kuzingatia kikamilifu taratibu na miongozo ya TSC, sambamba na maelekezo ya Serikali ya Awamu ya Sita," alisema Bw. Julius.

Katika kipindi hicho hicho, walimu 501 walisajjiwa rasmi baada ya kuajiriwa rasmi, walimu 404 walithibitishwa kazini baada ya kukidhi vigezo vinavyotakiwa, huku walimu 272 wakibadilishwa vyeo kulingana na sifa zao.



Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Tarime, Bw. Agutu Julius akiwa ofisini kwake.

Nidhamu Yaongezeka, Utoro Wapungua

Kwa upande wa nidhamu, TSC Tarime imefanikiwa kupunguza kwa kiasi kikubwa vitendo vya utoro kazini. Taarifa ilieleza kuwa mashauri ya nidhamu 64 yalishughulikiwa kati ya mwaka 2021 na 2025.

"Miaka ya nyuma tulikuwa tunapokea zaidi ya kesi 20 za utoro kwa mwaka, lakini kwa sasa tunapokea chini ya kesi 10 kwa mwaka," alifafanua Bw. Julius, akibainisha kuwa hali hiyo ni matokeo ya elimu na usimamizi madhubuti.

Aliongeza kuwa utoaji wa miongozo na maelekezo kutoka TSC Makao Makuu umeongeza uelewa

kwa walimu kuhusu sheria, kanuni na taratibu za utumishi wao.

Ziara Za Elimu Ya Utumishi Zatoa Matokeo

Katika juhudi za kuimarisha maadili na uwajibikaji, TSC Tarime imefanya ziara maalum shuleni kwa lengo la kutoa elimu ya utumishi. Kupitia ziara hizo, walimu 1,926 wamepatiwa elimu kuhusu haki, wajibu na maadili ya kazi kati ya mwaka 2021 na 2025.

"Ziara hizi zimetusaidia kuwajengea walimu uelewa mpana wa majukumu yao na kuwahamasisha kuzingatia misingi ya utumishi wa umma," alisema Bw. Julius.

Mafunzo Elekezi Yaimarisha Walimu Wapya

Aidha, kuanzia mwaka 2025, walimu wapya wanaopata mafunzo elekezi wamekuwa wakipatiwa vitabu vya mwongozo wa utumishi, hatua inayolenga kuwawezesha kuanza kazi wakiwa na uelewa sahihi wa mifumo ya kazi.

Bw. Julius alisema kuwa mafunzo hayo yamewasaidia walimu wapya kutambua haki na wajibu wao, pamoja na tahadhari dhidi ya vitendo vinavyoweza kuhatarisha taaluma yao.

"Mafunzo haya yamechangia kwa kiasi kikubwa kuongeza nidhamu, ufanisi na uwajibikaji miongoni mwa walimu wapya," alisisitiza.



Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Tarime, Bw. Elihudi Joseph Chogo (kushoto) pamoja na Bw. Agustino Abdallah wakiwa kwenye kikao na Maafisa kutoka Kitengo cha Mawasiliano Serikalini cha TSC (hawapo pichani) katika ofisi za Tume Wilaya ya Tarime hivi karibuni.

TSC TARIME YANG'ARA: WALIMU ZAIDI YA 3,000 WAPANDISHWA VYEO NDANI YA MIAKA MINNE



Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Tarime, Bi. Sophia Aoko Alfred (kushoto) pamoja na Bw. Elihudi Joseph Chogo wakiwa kwenye kikao na Maafisa kutoka Kitengo cha Mawasiliano Serikalini cha TSC (hawapo pichani) katika ofisi za Tume Wilaya ya Tarime hivi karibuni.



Picha ya pamoja ya watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Tarime.

TUME YA UTUMISHI WA WALIMU MAGU YAISHUKURU SERIKALI KWA KUONDOA KERO ZA WALIMU

Na Mwandishi Wetu – Magu

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Magu imeishukuru Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kufanikiwa kuondoa changamoto ya muda mrefu ya walimu kutopandishwa vyeo kwa wakati.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Magu, Bi. Emmanuela Peter, wakati akizungumza na Maafisa Habari wa Tume ya Utumishi wa Walimu kutoka Makao Makuu kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2021 hadi 2025.

Bi. Emmanuela alisema kuwa hatua ya Serikali ya kuwapandisha walimu vyeo na kupunguza mrundikano wa walimu waliokuwa hawajapandishwa kwa muda mrefu imechangia kwa kiasi kikubwa kupunguza malalamiko na kuongeza morali ya kazi kwa walimu.

“Tunamshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa jitihada kubwa alizozifanya katika kutatua kero za walimu, ikiwemo masuala ya madaraja, kubadilishiwa miundo ya utumishi, kulipa malimbikizo ya mishahara na madai ya nuli. Hali ya upandishaji wa vyeo na madaraja kwa sasa ni nzuri na inaridhisha. Serikali imesikiliza kilio cha walimu na kuwapa faraja,” alisema.

Alisema kuwa katika kipindi hicho, walimu 2,315 wamepandishwa vyeo, huku walimu 411 wakibadilishiwa miundo ya utumishi baada ya kujiendeleza kielimu. Aliongeza kuwa zoezi la upandishaji vyeo kwa walimu wa Wilaya ya Magu lilifanyika kwa kuzingatia muda wa utumishi, bila kuathiri tarehe halisi za kupanda madaraja wala nyongeza ya mishahara.

Bi. Emmanuela aliwataka walimu kuendelea kufanya kazi kwa bidii, uadilifu na kuzingatia maadili na miiko ya utumishi wa umma, hasa baada ya Serikali kushughulikia changamoto zao kwa kiasi kikubwa.

Aidha, alisema kuwa katika kipindi hicho Serikali imelipa walimu 818 malimbikizo ya mishahara, na walimu 1,534 kutoka Idara ya Elimu ya Awali na Msingi wamelipwa madai ya likizo.

Katika hatua nyingine, Kaimu Katibu Msaidizi huyo aliishukuru Serikali kwa uboreshaji wa miundombinu ya elimu, ikiwemo ujenzi wa shule mpya na nyumba za kisasa za walimu, hatua ambayo imeongeza ari ya walimu kufundisha na wanafunzi kujifunza. Alisema ujenzi wa shule mpya umepunguza mrundikano wa wanafunzi madarasani, huku matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) yakiboresha ufundishaji na ujifunzaji.

Wakati huo huo, Bi. Emmanuela alisema kuwa miongozo iliyotolewa hivi karibuni na Tume ya Utumishi wa Walimu imewasaidia walimu kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma na kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia maadili ya kazi.

Aliongeza kuwa kupitia miongozo na machapisho mbalimbali, TSC Wilaya ya Magu kwa kushirikiana na

Ofisi ya Mkurugenzi imekuwa ikifanya ziara katika vituo vya kazi vya walimu kwa lengo la kuwakumbusha Sheria, Kanuni, Taratibu na Maadili ya utumishi, hatua inayolenga kuwajenga walimu kuwa kioo cha jamii.

Kwa upande wao, baadhi ya walimu katika Wilaya ya Magu wameishukuru Serikali kwa kutoa kipaumbele katika utatuzi wa changamoto zao na kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji.

Mwalimu Doroth Mussa Bukangowa wa Shule ya Msingi Salisima alisema, Serikali ya Awamu ya Sita imejitahidi kuboresha maslahi ya walimu pamoja na mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Alisema matumizi ya mifumo ya TEHAMA shuleni yamepunguza gharama za uendeshaji, kurahisisha mawasiliano na kuboresha utoaji wa elimu.

Aliomba Serikali kuendelea kuongeza idadi ya walimu na vitabu kwa kila mwanafunzi ili kuboresha zaidi utekelezaji wa majukumu ya walimu.

Naye Mwalimu Pascally Maingu Mlemela wa Shule ya Sekondari Masengesa alisema, Serikali inaendelea kufanya kazi nzuri katika kuboresha maslahi ya walimu. Alishauri upandishwaji wa madaraja ufanyike moja kwa moja kupitia mfumo, pamoja na maboresho ya muundo wa vyeo kwa walimu ajira mpya kulingana na sifa zao za kitaaluma.

Aidha, aliipongeza Serikali kwa kutoa miongozo kupitia Tume ya Utumishi wa Walimu, akisema imesaidia kutoa elimu ya kujitambua na kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma. Aliongeza kuwa utekelezaji wa mitaala mipya umeboresha ufundishaji kwa kuzingatia vitendo zaidi kuliko nadharia, na kurahisisha utoaji wa elimu ikilinganishwa na mitaala ya awali.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Magu, Bi. Emmanuela Peter, akizungumza na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita.

**TUME YA UTUMISHI WA WALIMU MAGU YAISHUKURU
SERIKALI KWA KUONDOA KERO ZA WALIMU**

Bi. Emmanuela Peter (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Maafisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Magu.

MIONGOZO YA TSC YAPUNGUZA UTORO KWA WALIMU WILAYANI GEITA

Na Mwandishi Wetu – Geita

Miongozo mbalimbali iliyotolewa hivi karibuni na Serikali kupitia Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza tatizo la utoro kwa walimu katika Wilaya ya Geita.

Kauli hiyo imetolewa na Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Geita, Bw. Magina Mandago Egata, wakati wa mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Makao Makuu, alipokuwa akieleza mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kuwatumikia walimu.

Bw. Egata alisema kuwa kupitia miongozo hiyo, matukio ya utoro kwa walimu yamepungua kutoka wastani wa walimu 12 kwa robo ya mwaka 2022/2023 hadi kufikia walimu 4 pekee kwa robo ya mwaka 2023/2024.

Aliongeza kuwa walimu wameanza kutambua haki na wajibu wao kwa mwajiri, wanafunzi na jamii kwa ujumla katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

Aidha, alisema kuwa ofisi yake imekuwa ikiendesha mafunzo na semina elekezi kwa walimu kwa lengo la kuboresha utendaji kazi na kuwajengea uelewa wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wao, hatua inayowasaidia kuepuka vitendo vinavyoweza kuhatarisha ajira zao.

Katika hatua nyingine, Bw. Egata alisema kuwa jumla ya walimu 3,879 wa Wilaya ya Geita wamepandishwa madaraja kuanzia mwaka 2022 hadi 2025, ambapo walimu wa shule za msingi ni 2,822 na walimu wa shule za sekondari ni 1,057.

Kwa upande wao, walimu wa Wilaya ya Geita wameipongeza Serikali kwa kuboresha maslahi yao na kutatua changamoto zilizokuwa zikiwakabili kwa muda mrefu, hali iliyochangia kuongeza morali ya utoaji elimu.

Mkuu wa Shule ya Msingi Nyanza, Mwl. Bernadether Mashine, alisema kuwa jitihada za Serikali kuhakikisha walimu waliokuwa hawajapandishwa madaraja kwa muda mrefu wanapata stahiki zao sasa zinaonekana wazi.

Alisema kuwa Serikali imeweka mfumo unaohakikisha kila mwalimu anapandishwa daraja kulingana na sifa alizonazo na muda wa utumishi wake.

Aidha, aliongeza kuwa Serikali imeboresha miundombinu ya elimu kwa kujenga shule mpya, ikiwemo Shule ya Msingi Moringe, hatua iliyosaidia kupunguza msongamano wa wanafunzi katika shule yake.

Mwl. Mashine aliipongeza Serikali kwa kuanzisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utoaji wa elimu, akisema kuwa yamewaongezea maarifa walimu na wanafunzi.

Naye Mwl. Christophina Raphael Kisenga aliishukuru Serikali kwa kumtatulia changamoto ya kukaa katika daraja moja kwa muda mrefu, hali iliyosababisha kupandishwa madaraja mara mbili na sasa anatarajia kupanda tena mwaka 2027.

Alisema kuwa matumizi ya TEHAMA yamewasaidia walimu kujengeana uwezo kwa kubadilishana mawazo



Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Geita Bw. Magina Mandago Egata akiwa katika mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Makao Makuu kuelezea kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kuwatumikia walimu.

kuhusu mada mbalimbali wanazofundisha pamoja na kupunguza urasimu katika huduma kama mikopo, uhamisho na likizo.

Kwa upande wake, Mwl. Deogratius Anthony Kagoma alisema kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imerejesha matumaini yake baada ya tatizo la kuchelewa kupandishwa madaraja kutatuliwa, jambo lililokuwa likimkatisha tamaa kwa muda mrefu.

Makamu Mkuu wa Shule ya Sekondari Geita, Mwl. Straton Thomas, alisema kuwa Serikali imehakikisha kila mwalimu anapata haki yake kwa wakati kupitia uboreshaji wa mfumo wa upimaji wa watumishi kwa njia ya mtandao.

Aliongeza kuwa matumizi ya TEHAMA yamewasaidia walimu kuongeza ujuzi na kubadilishana uzoefu, hali inayowanufaisha moja kwa moja wanafunzi.

Naye Mwl. Stephen Richard Ngodoki aliishukuru Serikali kwa kuboresha maslahi ya walimu, ikiwemo nyongeza ya mishahara na upandishwaji wa madaraja, pamoja na kuweka dirisha la mikopo kupitia mifumo rasmi, hatua iliyopunguza urasimu.

Kwa upande wake, Mwl. Batano James alisema kuwa ajira mpya za walimu zimepunguza mzigo wa ufundishaji, hasa katika madarasa yenye idadi kubwa ya wanafunzi.

Aliongeza kuwa Serikali imeboresha miundombinu ya elimu kwa kujenga vyumba vya madarasa, mabweni, maabara za sayansi pamoja na kutoa vifaa vya maabara, hali iliyoboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji.

MIONGOZO YA TSC YAPUNGUZA UTORO KWA WALIMU WILAYANI GEITA



Mkuu wa Shule ya Msingi Nyanza Mwl. Bernadether Mashine akiwa katika mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Marwasiliano Makao Makuu kuelezea kuhusu mafanikio ya Serikali ya Azwamu ya Sita katika kuwatumikia walimu.



Mkuu wa Shule ya Msingi Nyanza Mwl. Bernadether Mashine akiwa katika mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Marwasiliano Makao Makuu kuelezea kuhusu mafanikio ya Serikali ya Azwamu ya Sita katika kuwatumikia walimu.



Mwalimu wa Shule ya Msingi Nyanza Mwl. Christophina Raphael Kisenga Mwalimu wa Shule ya Msingi Nyanza Mwl. Deogratius Anthony Kagoma akiwa katika mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Marwasiliano Makao Makuu kuelezea kuhusu mafanikio ya Serikali ya Azwamu ya Sita katika kuwatumikia walimu.



Makamu Mkuu wa Shule ya Sekondari Geita Mwl. Straton Thomas akiwa katika mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Marwasiliano Makao Makuu kuelezea kuhusu mafanikio ya Serikali ya Azwamu ya Sita katika kuwatumikia walimu.



Mwalimu katika Shule ya Sekondari Geita Mwl. Stephen Richard Ngodiki akiwa katika mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Marwasiliano Makao Makuu kuelezea kuhusu mafanikio ya Serikali ya Azwamu ya Sita katika kuwatumikia walimu.



Mwalimu katika Shule ya Sekondari Geita Mwl. Batano James akiwa katika mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Marwasiliano Makao Makuu kuelezea kuhusu mafanikio ya Serikali ya Azwamu ya Sita katika kuwatumikia walimu.

MIAKA MITANO YA MAFANIKIO YA TSC BUNDA KATIKA KUTATUA KERO ZA WALIMU

**Na Mwandishi wetu – Bunda,
Mara.**

Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Bunda imeendelea kuonesha mafanikio makubwa katika kushughulikia masuala ya walimu kuanzia mwaka 2021 hadi 2025, hali iliyochangia kuimarika kwa mazingira ya kazi, nidhamu na ubora wa elimu wilayani humo.

Akizungumza katika mahojiano maalum na Jarida la Sauti ya TSC, Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Bunda, Bw. Sinda Maji John, alisema ofisi hiyo imeweka mkazo katika ajira, maadili na maendeleo ya walimu pamoja na utatuzi wa changamoto zao.

Bw. Sinda alisema katika kipindi cha miaka mitano, walimu 425 waliajiriwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda na Halmashauri ya Mji wa Bunda, hatua ilipunguza kwa kiasi kikubwa uhaba wa walimu shuleni na kuongeza ufanisi wa utoaji wa elimu.

Kwa upande wa maendeleo ya watumishi, jumla ya walimu 3,750 walipandishwa madaraja kwa wakati, wakiwemo walimu 1,012 waliopandishwa kwa msererereko. Hatua hiyo imeelezwa kuondoa malalamiko ya muda mrefu na kuongeza morali na ari ya kazi kwa walimu.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Bunda, Bw. Sinda Maji John akitoa ufafanuzi wakati wa mahojiano maalum na Jarida la Sauti ya TSC ofisini kwake hivi karibuni.

Aidha, walimu 345 waliokuwa wamejiendeleza kielimu wamebadilishiwa miundo ya kiutumishi kwa wakati, huku walimu 215 wakithibitishwa kazini baada ya kuonesha uwezo na nidhamu bora. Walimu 127 walipewa vibali vya kustaafu kazi kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratizu za Utumishi wa Umma.

Kuhusu kero za walimu, ofisi ya TSC Wilaya ya Bunda ilianzisha

kliniki za ndani kwa kushirikiana na Idara za Utumishi na Elimu, hatua iliyosaidia kubaini na kushughulikia ucheleweshaji wa madaraja, miundo na malimbikizo ya mishahara kwa walimu 233.

Changamoto ya ucheleweshaji wa fedha za likizo nayo imeendelea kufuatiliwa kwa karibu, ambapo baadhi ya walimu wameshalipwa na wengine wameahidiwa kulipwa kupitia bajeti za halmashauri.

Katika kuimarisha nidhamu ya walimu, Bw. Sinda alisema mafunzo na miongozo ya hivi karibuni iliyotolewa na TSC Makao Makuu imeleta matokeo chanya, kwani idadi ya mashauri ya nidhamu imepungua kutoka kesi 22 mwaka 2021 hadi kesi 8 mwaka 2025.

Aliongeza kuwa ufanisi wa TSC Bunda umechangiwa pia na uwezeshwaji wa vitendea kazi, mafunzo ya watumishi, vikao vya kisheria na ushirikiano mzuri na wadau wa elimu wilayani humo.

Bw. Sinda alihitimisha kwa kusema kuwa mafunzo elekezi kwa walimu wapya yamewasaidia kutambua haki, wajibu na maadili ya utumishi tangu kuajiriwa, hali inayochangia taswira chanya ya walimu na kuimarika kwa elimu katika Wilaya ya Bunda.



Mmoja wa watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Bunda, Edward Ntungi akiwa ofisini kwake hivi karibuni.

TSC SERENGETI YAIMARISHA HUDUMA, WALIMU AJIRA MPYA WAPATA MAFUNZO MAALUMU

"Elimu ni ufunguo wa maendeleo; tunahakikisha walimu wanajua haki, wajibu na maadili yao, na tunashughulikia kila changamoto ili walimu wa Serengeti wafanye kazi zao kwa ufanisi," Bw. Mathias Kahazi Musabwa, Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Serengeti.



hadi 2025, walimu 2,347 wamepandishwa madaraja, wengi wakiwa wamepandishwa zaidi ya mara moja, malimbikizo ya mishahara kwa walimu 25 yamelipwa na walimu 405 wamesajiliwa na kuthibitishwa kazini.

Bw. Musabwa alisema kuwa mafunzo elekezi yamesaidia zaidi ya walimu 90 walioajiriwa mwaka 2025 kutimiza majukumu yao bila changamoto ya nidhamu.

"Aidha, walimu wameweza kutambua mipaka ya uwalimu, haki zao za kupata madai ya fedha na malimbikizo ya mishahara, na jinsi ya kuzingatia maadili kazini," alisema Bw. Musabwa.

Aliongeza kuwa, "Miongozo iliyotolewa na Tume Makao Makuu imewasaidia walimu kuepuka makosa ya nidhamu na kuongeza uwajibikaji wao kazini. Tofauti na kipindi cha awali ni kubwa, ambapo walimu walikumbwa na makosa kutokana na uelewa mdogo wa sheria na taratibu za utumishi."

Kwa jitihada hizi, TSC Wilaya ya Serengeti inaendelea kushughulikia masuala yote ya walimu, kuhakikisha nidhamu, maadili, na haki zao zinalindwa, huku ikichangia kuboresha utendaji kazi wa walimu katika shule za msingi na sekondari wilayani.

Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Serengeti, Bw. Mathias Musabwa akizungumza juu ya mafanikio ya ofisi hiyo katika kutoa huduma kwa walimu hivi karibuni.

Na Mwandishi wetu – Serengeti, Mara.

Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Serengeti inaendelea kuboresha huduma kwa walimu wote wilayani, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu yake kwa kipindi cha mwaka 2021 hadi 2025.

Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya, Bw. Mathias Musabwa, ameeleza kuwa jitihada hizi zinahusisha kutoa elimu kwa walimu kuhusu haki, wajibu, maadili ya utumishi, na kushughulikia changamoto zinazowakabili walimu katika shule za msingi na sekondari.

Wilaya ya Serengeti ina shule 166, ambazo ni shule 127 za msingi na 39 za sekondari, na ina walimu 1,823. Ofisi ya TSC Wilaya imetumia mbinu mbalimbali kuboresha utendaji kazi wa walimu, ikiwemo: kutoa mafunzo elekezi kwa walimu wapya, kufanya ziara za ngazi ya kata na shule kushiriki makongamano ya walimu na kutoa mada za Sheria, Kanuni, na Taratibu, pamoja na kusambaza nakala za miongozo mbalimbali kwa walimu.

Kwa mujibu wa kiongozi huyo kati ya mwaka 2021



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Serengeti, Bw. Mathias Musabwa akionesha vitabu alivyotumia katika kutoa mafunzo kwa walimu wa ajira mpya.

TSC SERENGETI YAIMARISHA HUDUMA, WALIMU AJIRA MPYA WAPATA MAFUNZO MAALUMU



Mtumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Serengeti, Mwl. John Joseph Malagira, akitoa mada katika mafunzo ya walimu ajira mpya mwaka 2025.



Mtumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Serengeti, Mwl. John Joseph Malagira akiendelea kutekeleza majukumu yake hivi karibuni.



Mtumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Serengeti, Malima Mgeta Charles akiendelea kutekeleza majukumu yake hivi karibuni.



Mtumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Serengeti, Wilson Hilary Chale akiendelea kutekeleza majukumu yake hivi karibuni.



Watumishi wa TSC Wilaya ya Serengeti wakirwa katika picha ya pamoja na walimu waliotembelea ofisi hiyo hivi karibuni.

ZAIDI YA WALIMU 700 WAMEAJIRIWA WILAYANI CHATO

Na Mwandishi Wetu – Chato

Serikali imeajiri jumla ya walimu 732 katika Wilaya ya Chato katika kipindi cha kuanzia mwaka 2021 hadi 2025.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Chato, Bw. Vedastus Msiba, wakati akielezea mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kuwatumikia walimu.

Bw. Msiba alisema kuwa kati ya walimu hao, walimu wa shule za msingi ni 354 huku walimu wa shule za sekondari wakiwa 378.

Aidha, alisema kuwa katika kipindi hicho kuanzia mwaka 2021 hadi 2025, Serikali imewapandisha vyeo walimu 5,645, ambapo walimu

wa shule za msingi walikuwa 4,341 na walimu wa shule za sekondari 1,304.

Aliongeza kuwa walimu 494 wamebadilishiwa cheo baada ya kujiendeleza kielimu, kati yao walimu wa shule za msingi wakiwa 439 na wa shule za sekondari 55.

Bw. Msiba aliishukuru Serikali kwa kuchapisha miongozo mbalimbali na kutoa maelekezo ambayo yamesaidia walimu kuelewa Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia utumishi wao.

“Hili limewasaidia walimu kutambua makosa ya kinidhamu pamoja na mamlaka za kinidhamu kuanzia ngazi ya shule hadi ngazi ya kitaifa. Tofauti na siku za nyuma, makosa ya kinidhamu yalikuwa mengi,” alisema.

Alifafanua kuwa kupitia Mwongozo wa Mafunzo Elekezi, walimu wapya wamejengewa uelewa kuhusu haki zao ikiwemo malipo ya mishahara, likizo, matibabu na masuala ya malezi, pamoja na kuwafahamisha wajibu wao wa kuhudhuria kazini, kuandaa masomo na kuheshimu kanuni za utumishi wa umma.

Bw. Msiba alisema kuwa mwaka 2024, Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Chato ilirekodi makosa ya kinidhamu 36, huku mwaka 2025 idadi hiyo ikipungua na kufikia 17 pekee.

Aliongeza kuwa ofisi hiyo imekuwa ikiendesha ziara za mara kwa mara kwa walimu kupitia semina za maadili, warsha za elimu ya nidhamu na utendaji kazi, pamoja na mikutano ya walimu na uongozi wa shule kwa lengo la kujadili sheria mpya, taratibu na mabadiliko ya sera.

Wakati huo huo, walimu wa Shule ya Sekondari ya Wema wilayani Chato wameipongeza Serikali kwa kuboresha maslahi yao na kutatua changamoto zilizokuwa zikiwakabili kwa mudamrefu, ikiwemo kuchelewa kwa nyongeza za mishahara na upandishwaji wa madaraja.

Walisema kuwa Serikali imejitahidi kuhakikisha walimu waliokuwa hawajapandishwa vyeo kwa muda mrefu wanapandishwa kwa wakati na kuwekwa katika madaraja wanayostahili.

“Kwa sasa Serikali inawapandisha walimu madaraja kwa wakati, imeongeza mishahara na kuboresha maslahi kwa ujumla,” walisema.

Waliongeza kuwa katika kuimarisha maendeleo ya sayansi na teknolojia, Serikali imejenga maabara za kisasa za masomo ya Kemia, Fizikia na Baiolojia, hali inayowawezesha wanafunzi kujifunza kwa vitendo badala ya nadharia pekee.

Aidha, walisema kuwa Serikali imeendelea kujenga shule mpya ili kupunguza msongamano wa wanafunzi katika shule zilizopo na kuweka mazingira bora ya ufundishaji na ujifunzaji.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Chato, Bw. Vedastus Msiba, (upande wa kulia) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa Tume Wilaya ya Chato.

ZAIDI YA WALIMU 700 WAMEAJIRIWA WILAYANI CHATO



MWALIMU BERNARD PAUL NGERO AIPONGEZA SERIKALI YA AWAMU YA SITA KWA KUBOresha MASLAHI NA MAZINGIRA YA KAZI YA WALIMU

Na Mwandishi wetu – Bunda, Mara.

Mwalimu Bernard Paul Ngero, mwalimu wa Shule ya Awali na Msingi Azimio Bunda, ameipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa jitihada kubwa inazoendelea kuzifanya katika kuboresha maslahi ya walimu na sekta ya elimu kwa ujumla.

Akizungumza katika mahojiano maalum, Mwalimu Ngero amesema kuwa juhudi za serikali katika masuala ya mishahara, madaraja na mazingira ya kazi zimeleta matumaini mapya kwa walimu nchini, tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma.

“Kwa mtazamo wangu binafsi, jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita ni kubwa mno. Maslahi ya walimu yamepewa kipaumbele cha kweli,” amesema.

Ameeleza kuwa nyongeza za mishahara zinazofanyika kila mwaka zimewasaidia walimu kukabiliana na changamoto za maisha ya kila siku kutokana na mabadiliko ya kiuchumi. Aidha, suala la kupandishwa madaraja sasa linafanyika kwa wakati, jambo lililokuwa changamoto kubwa kwa muda mrefu.

“Zamani kupanda daraja ilikuwa kama bahati ya mtu binafsi, lakini sasa walimu wanaostahili wanapandishwa kwa wakati,” alisisitiza.

Kwa upande wa mazingira ya kazi, Mwalimu Ngero amesema serikali imefanya mapinduzi makubwa kwa kujenga na kukarabati miundombinu ya shule, ikiwemo madarasa, ofisi, vyoo pamoja na nyumba bora za walimu. Shule ya Msingi Azimio Bunda ni miongoni mwa shule mpya za kisasa zilizojengwa na Serikali ya Awamu ya Sita na kuanza rasmi Januari 2024.

Katika ushuhuda wake binafsi, Mwalimu Ngero amesema yeye ni mnufaika wa moja kwa moja wa juhudi hizo baada ya kupandishwa daraja kutoka Mwalimu Mwandamizi Daraja C kwenda Mwalimu Mkuu Daraja II C Julai 2024.

Ameongeza kuwa mafanikio ya sekta ya elimu yameonekana wazi kupitia kuongezeka kwa ari ya kazi miongoni mwa walimu, ufanisi katika ufundishaji, pamoja na kuongezeka kwa ufaulu wa wanafunzi mwaka hadi mwaka.

“Walimu sasa wanachapa kazi kwa bidii kwa sababu kilio chao kimesikilizwa. Sekta ya elimu imekuwa ya kuheshimika zaidi,” amesema.

Kuhusu matumizi ya mifumo ya TEHAMA, amesema yameongeza ufanisi, yamepunguza urasimu, gharama za uendeshaji wa shule na kuwawezesha walimu kuwa mahiri zaidi kiteknolojia, hasa katika mawasiliano na usimamizi wa rasilimali.

Aidha, ameipongeza serikali kwa kuanzisha mitaala mipya ya elimu inayomlenga mwanafunzi, inayojenga umahiri, maadili, uzalendo na elimu jumuishi kwa watoto

wote wakiwemo wenye mahitaji maalum.

Hata hivyo, ameshauri serikali kuendelea kuziwezesha shule vifaa vya TEHAMA, kuwajengea walimu uwezo zaidi, pamoja na kutoa elimu kwa jamii kuhusu mabadiliko ya mitaala hiyo.

“Kwa ujumla, Serikali ya Awamu ya Sita imeigusa sekta ya elimu kwa kiwango kikubwa sana. Kongole kwa serikali,” alihitimisha Mwalimu Ngero.



Mwl. Bernard Paul Ngero wa Shule ya Awali na Msingi Azimio Bunda akitoa maelezo wakati wa mahojiano maalum na Jarida hili hivi karibuni.

SERIKALI YAENDELEA KUBORESHA MASLAHI, NIDHAMU NA MAZINGIRA YA KAZI KWA WALIMU RORYA

Na Mwandishi wetu – Rorya, Mara.

Serikali kupitia Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Rorya imeendelea kutekeleza maboresho makubwa katika masuala ya ajira, maslahi na nidhamu kwa walimu, hatua inayolenga kuinua ubora wa elimu na kuimarisha ustawi wa walimu katika wilaya hiyo.

Akizungumza na Jarida la Sauti ya TSC ofisini kwake hivi karibuni, Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Rorya, Charwi John, alisema kuwa Serikali imedhamiria kuhakikisha walimu wanalindwa, wanawezeshwa na wanatekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

“Katika kipindi cha mwaka 2021 hadi 2025, Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Rorya imehakikisha walimu wanapata haki zao kwa wakati, kuanzia usajili, kuthibitishwa kazini, upandishaji vyeo pamoja na kushirikiana na mamlaka zingine kuhakikisha stahiki mbalimbali zinalipwa,” alisema Charwi.

Kwa mujibu wa Charwi, TSC Wilaya ya Rorya inahudumia jumla ya walimu 1,709 wanaofundisha katika shule 183 za serikali, zikiwemo shule za msingi 134 na sekondari 49. Katika kipindi hicho, walimu 432 wamesajiliwa, huku walimu 469 wakithibitishwa kazini.

Aliongeza kuwa walimu 1,729 wamepandishwa vyeo, huku walimu 142 waliokuwa wamechelewa kupanda wakipandishwa kwa mserereko.

“Hatua hizi zimeleta faraja kubwa kwa walimu na kuongeza morali ya kazi, jambo linalochangia moja kwa moja kuboresha ufundishaji na ujifunzaji shuleni,” alifafanua.

Katika kuboresha maslahi ya walimu, Charwi alisema Serikali imeendelea kushughulikia madai ya malimbikizo ya mishahara, ambapo madai ya walimu 793 yalipokelewa na walimu 416 tayari wamelipwa, huku taratibu za malipo kwa waliobaki zikiendelea.

“Ofisi yetu imeendelea kuwezeshwa kutekeleza majukumu

yake kwa ufanisi zaidi, ambapo watumishi wa Tume pamoja na wajumbe wa Kamati ya Ajira, Upandishwaji Vyeo na Nidhamu wamepatiwa mafunzo ya mara kwa mara,” alisema.

Charwi alisema miongozo mbalimbali iliyotolewa na Tume imechangia kwa kiasi kikubwa kuimarisha nidhamu na kupunguza migogoro iliyokuwa ikijitokeza kati ya wakuu wa shule na walimu.

“Kuongezeka kwa uelewa wa sheria, kanuni na taratibu za utumishi kumeondoa migogoro mingi iliyokuwa inasababishwa na kutoelewana au kutokujua haki na wajibu,” alieleza.

Matokeo ya maboresho hayo yameonekana pia katika kupungua kwa mashauri ya kinidhamu, ambapo kuanzia mwaka 2021 hadi 2023, mashauri 24 yalipokelewa,

huku mwaka 2024 na 2025 mashauri matatu tu yameripotiwa.

Hata hivyo, Charwi alibainisha kuwa bado kuna changamoto chache zinazohitaji ushirikiano wa wadau, ikiwemo suala la baadhi ya walimu wachache kuwa na mikopo iliyopitiliza uwezo wao wa marejesho.

“Baadhi ya walimu wamechukua mikopo mikubwa kupita uwezo wao wa kulipa, hali inayosababisha usumbufu wa kudaiwa na wakati mwingine kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi,” alisema.

Alisisitiza kuwa Tume kwa kushirikiana na wadau wengine inaendelea kutoa elimu ya kifedha kwa walimu ili kuwasaidia kusimamia vyema mikopo yao na kuepuka athari zinazoweza kuathiri utendaji kazi na utoaji wa elimu.

Kwa ujumla, Charwi alisema maboresho hayo yanaonesha dhamira ya Serikali ya kuendelea kuimarisha mazingira ya kazi kwa walimu na kuhakikisha taaluma ya ualimu inaheshimiwa na kuchangia kikamilifu maendeleo ya elimu na taifa kwa ujumla.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Rorya Charwi John akizungumzia maendeleo ya walimu katika Wilaya hiyo hivi karibuni.

SERIKALI YAENDELEA KUBORESHA MASLAHI, NIDHAMU NA MAZINGIRA YA KAZI KWA WALIMU RORYA



Mtumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Rorya, Paul Amos akiwa ofisini kwake.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Rorywa Charwi John (kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na afisa wa TSC Wilaya ya Rorya, Bw. Paul Amos hivi karibuni.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Rorywa Charwi John (kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Tarime, Bw. Agutu Julius (kulia) na afisa wa TSC Wilaya ya Rorya, Bw. Paul Amos nje ya Ofisi za Tume Rorya.

SERIKALI IMEAJIRI WALIMU 155 WILAYANI NYANG'HWALE

**Na Mwandishi Wetu –
Nyang'hwale**

Serikali imeajiri na kuthibitisha kazini jumla ya walimu 155 wa shule za msingi na sekondari wilayani Nyang'hwale, mkoani Geita, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2021 hadi 2025.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Nyang'hwale, Bw. Shija Mapalala, wakati wa mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Makao Makuu kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kuwatumikia walimu.

Bw. Mapalala alisema kuwa katika kipindi hicho walimu 39 wa shule za msingi wameajiriwa na kuthibitishwa kazini, huku walimu 116 wa shule za sekondari nao wakiajiriwa na kuthibitishwa kazini.

Aliongeza kuwa mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na walimu 1,827 kupandishwa madaraja, ambapo walimu wa shule za msingi ni 1,382 na walimu wa sekondari ni 445. Aidha, walimu 137 walibadilishiwa miundo ya utumishi baada ya kujiendeleza kielimu.

"Tunaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kusikia kilio cha muda mrefu cha walimu. Walimu waliostahili wamepandishwa madaraja kwa haki zao. Kabla ya mwaka 2021, walimu wengi hawakuwa wakipandishwa vyeo kwa muda mrefu, hali iliyosababisha malalamiko mengi," alisema Bw. Mapalala.

Alisema hatua hiyo inathibitisha jitihada za Serikali kupitia Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Nyang'hwale katika kushughulikia kero za walimu kuanzia mwaka 2021 hadi 2025.

Aidha, aliishukuru Serikali kupitia TSC kwa kuandaa mafunzo elekezi kwa walimu wapya 112, yaliyolenga kuwajengea uwezo kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma ili kuwakinga dhidi ya kujiingiza kwenye mashauri ya kinidhamu yanayoweza kuhatarisha ajira zao.

Bw. Mapalala alisema kuwa kupitia mafunzo hayo na Mwongozo wa Mafunzo Elekezi waliopatiwa, walimu wapya wameweza kufahamu kwa kina sheria, kanuni na taratibu zinazowaongoza, pamoja na kutambua haki, stahiki na wajibu wao kwa mwajiri, wanafunzi na jamii kwa ujumla.

Aliongeza kuwa mwongozo huo umechangia kuwajengea walimu wapya uelewa wa haki zao, ikiwemo mishahara, likizo, matibabu na masuala ya malezi, sambamba na kuwajengea ufahamu wa wajibu wao wa kuhudhuria kazini, kuandaa masomo na kuheshimu kanuni za utumishi wa umma.

"Mwongozo huu umewasaidia sana walimu wapya kuelewa haki zao na namna ya kuzidai kwa kufuata maadili ya utumishi wa umma, huku ukiwajengea nidhamu katika utekelezaji wa majukumu yao," alisema.

Alisema mbali na kutoa mwongozo huo kwa walimu wapya, TSC Wilaya pia imekuwa ikifanya ziara za kutoa semina za maadili kwa walimu wote, warsha za elimu ya nidhamu na utendaji kazi, pamoja na mikutano ya mara kwa mara kati ya walimu na uongozi wa shule kujadili sheria, taratibu na mabadiliko ya sera.

Bw. Mapalala aliongeza kuwa ofisi hiyo pia hutumia matangazo na mabango ya TSC katika shule na ofisi mbalimbali kuwaelimisha walimu kuhusu miongozo mipya ya utumishi, sambamba na kushirikiana na taasisi nyingine za Serikali katika kutafsiri sheria, kusimamia utekelezaji wake na kutoa ushauri wa kitaaluma kwa walimu wanaokiuka maadili ya kazi.

Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Nyang'hwale inahudumia walimu 1,207, wakiwemo walimu 848 wa shule za msingi na walimu 359 wa shule za sekondari, wanaohudumia jumla ya shule 92, ambapo shule za msingi ni 74 na sekondari 18.



Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Nyang'hwale, Bw. Shija Mapalala, wakati wa mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Makao Makuu.



Afisa wa TSC Wilaya ya Nyang'hwale, Bw. George Johnson, akiendelea na majukumu yake ya kila siku.

SERIKALI IMEAJIRI WALIMU 155 WILAYANI NYANG'HWALE



Kiamu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Nyang'hwale, Bw. Shija Mapalala (wa kwanza kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na Watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale na Mtumishi wa TSC, Bw. George Johnson (wa kwanza upande wa kulia).



WALIMU WA SHULE YA MSINGI KHARUMWA WAISHUKURU SERIKALI KWA KUTATUA KERO ZA MUDA MREFU

Na Mwandishi Wetu

Baadhi ya walimu wa Shule ya Msingi Kharumwa wilayani Nyang'hwale wameishukuru Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutatua changamoto zao za muda mrefu, hususan suala la kucheleweshwa kwa upandishaji madaraja.

Mwalimu wa shule hiyo, Delyca Osward, alisema kuwa Serikali imejitahidi kuwapandisha walimu madaraja na kuwaweka katika nafasi sahihi wanazostahili kwa kipindi hiki, jambo lililoongeza morali ya kazi kwa walimu.

Aliongeza kuwa matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) shuleni yameleta mageuzi makubwa, kwani sasa taarifa nyingi hutumwa kupitia mifumo rasmi, na

kurejeshwa kwa maboresho pale panapobainika makosa.

"Tunaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuanzisha mitaala mipya inayohusisha vitendo zaidi. Mitaala hii imeongeza ushirikishwaji wa wanafunzi na kuwawezesha kuelewa vizuri badala ya kukariri," alisema.

Kwa upande wake, Mwalimu Sangu Charles alisema kuwa hatua ya kuondoa ucheleweshaji wa upandishaji madaraja ni mojawapo ya mafanikio makubwa ya Serikali ya Awamu ya Sita ambayo hayatasahaulika kwa walimu wengi.

Alisema kuwa kwa miaka mingi walimu walikuwa wakiumizwa na hali hiyo, jambo lililopunguza morali ya kazi, lakini kuanzia mwaka 2021 hadi 2025 Serikali imehakikisha walimu wanapandishwa madaraja kwa wakati unaostahili.

"Nilishindwa kuendelea na masomo ya shahada katika Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino (SAUT) kutokana na kuchelewa kupandishwa daraja, jambo lililonikatisha tamaa. Leo hali imebadilika," alisema.

Aliongeza kuwa uboreshaji wa miundombinu ya shule, ikiwemo ujenzi wa shule mpya na madarasa, umepunguza msongamano wa wanafunzi na kuboresha mazingira ya kazi kwa walimu.

Mwalimu huyo pia aliipongeza Serikali kwa kuanzisha mifumo ya TEHAMA ambayo imewawezesha walimu kunufaika na huduma za kifedha, ikiwemo mikopo, bila udhalilishaji uliokuwepo awali.

Mkuu wa Shule ya Msingi Kharumwa, Bw. Justine Charles Mathias, alisema kuwa kabla ya kutatuliwa kwa changamoto ya upandishaji madaraja, mazingira ya uongozi shuleni yalikuwa magumu kutokana na malalamiko ya walimu, lakini sasa hali imeimarika na mahusiano yamekuwa rafiki zaidi.



Baadhi ya walimu wa Shule ya Msingi Kharumwa wilayani Nyang'hwale wakiwa katika picha ya pamoja na Afisa Elimu Kata, Bw. Petro Lucas Paul, mara baada ya mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini.

TUME YA UTUMISHI WA WALIMU WILAYA YA MBOGWE YAWEKEZA NGUVU ZAIDI KUZUIA MAKOSA YA KINIDHAMU KWA WALIMU

Na Mwandishi Wetu – Mbogwe

Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Mbogwe mkoani Geita imeendelea kuwekeza nguvu zaidi katika kuwajengea walimu uelewa wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma, hatua inayolenga kuwazuia kujiingiza katika vitendo vinavyoshusha hadhi ya taaluma ya ualimu na kuhatarisha ajira zao.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Mbogwe, Bi. Tamasha Masaza, wakati wa mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Makao Makuu, alipokuwa akielezea mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kuwatumikia walimu.

Bi. Tamasha alisema kuwa mbinu zinazotumika katika utoaji wa elimu kwa walimu ni pamoja na semina za maadili, mafunzo ya Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma, warsha za elimu ya nidhamu na utendaji kazi, pamoja na mikutano ya mara kwa mara kati ya walimu na uongozi wa shule kwa lengo la kujadili sheria mpya, taratibu na mabadiliko ya sera.

Aliongeza kuwa Tume pia hutumia matangazo na mabango rasmi ya Tume ya Utumishi wa Walimu yanayobandikwa katika shule na ofisi mbalimbali ili kuwaelimisha walimu kuhusu miongozo mipya.

Aidha, alisema kuwa ofisi hiyo hushirikiana na vyombo vya kusimamia na kutafsiri sheria kwa ajili ya kutoa ushauri wa kitaaluma kwa walimu wanaojikuta wakikiuka nidhamu ya kazi.

Bi. Tamasha alisema kuwa hatua hizo zimechangia kupungua kwa mashauri ya kinidhamu dhidi ya walimu kutoka mashauri 17 mwaka 2021 hadi kufikia mashauri 10 mwaka 2025.

Katika hatua nyingine, alisema kuwa katika kipindi cha kuanzia mwaka 2021 hadi 2025, jumla ya walimu 1,430 wa Wilaya ya Mbogwe wamepandishwa vyeo, ambapo walimu wa shule za msingi walikuwa 1,235 na walimu wa shule za



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Mbogwe, Bi. Tamasha Masaza, wakati wa mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Makao Makuu kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kuwatumikia walimu.

sekondari 195.

“Tunaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kusikiliza kilio cha muda mrefu cha walimu. Takwimu hizi zinaonesha kuwa walimu wote waliostahili kupandishwa vyeo wamepandishwa kulingana na sifa zao, tofauti na miaka ya nyuma kabla ya mwaka 2021 ambapo walimu wengi walichelewa kupandishwa na kusababisha malalamiko,” alisema.

Aliongeza kuwa hatua hiyo inathibitisha kuwa Serikali kupitia Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Mbogwe imefanikiwa kushughulikia kero nyingi za walimu katika kipindi cha kuanzia mwaka 2021 hadi 2025.

Bi. Tamasha alisema kuwa katika kipindi hicho, ofisi ilipokea kero 120 zinazohusu kucheleweshwa kwa upandishwaji wa madaraja, ambapo zote zilifanikiwa kushughulikiwa kwa kushirikiana na Tume ya Utumishi wa Walimu.

Kwa upande wa kero za kubadilishiwa miundo ya kiutumishi, alisema walipokea 85, ambapo 67 tayari zimeshughulikiwa na 18 zipo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji.

Aidha, alisema kuwa Serikali

imeendelea kupunguza tatizo la upungufu wa walimu kwa kuajiri walimu 488 katika Wilaya ya Mbogwe, wakiwemo walimu 300 wa shule za msingi na walimu 188 wa shule za sekondari.

Wakati huo huo, Bi. Tamasha alisema kuwa utoaji wa Mwongozo wa Mafunzo Elekezi (Induction Training Manual) kwa walimu wapya kupitia Tume ya Utumishi wa Walimu umeleta mchango mkubwa katika kuzuia mashauri ya kinidhamu kwa waajiriwa wapya.

Alifafanua kuwa mwongozo huo umewajengea walimu wapya uelewa wa haki zao ikiwemo mishahara, likizo, matibabu na masuala ya malezi, pamoja na kuwafahamisha wajibu wao wa kuhudhuria kazi, kuandaa masomo na kuheshimu kanuni za utumishi wa umma.

Bi. Tamasha alisema kuwa mafunzo hayo pia yameimarisha maadili ya utumishi kwa kuzingatia uadilifu, uwajibikaji, uaminifu na nidhamu, hali iliyoweka msingi imara wa utendaji kazi bora na kuzuia ukiukwaji wa sheria.

Aliongeza kuwa tangu kuanza kwa utoaji wa mafunzo hayo, hakuna kesi za kinidhamu zilizohusisha walimu wapya.

Kwa sasa, Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Mbogwe inawahudumia jumla ya walimu 1,438, wakiwemo walimu wa shule za msingi 1,044 na walimu wa shule za sekondari 394, wanaohudumia shule 97 za msingi na shule 22 za sekondari.



Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Mbogwe, Bw. Allen Nnko Daniel, akiendelea na majukumu yake ya kila siku wilayani humo.



MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu